



# KANUNI ZA USHIRIKI KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM (DITF)



## MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA

# KANUNI ZA USHIRIKI KATIKA MAONESHO YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM (DITF)

Kanuni za ushiriki wa maonesho zinatoa miongozo na utaratibu zinazoyakiwa kufuatwa na washiriki. Utekelezaji wa kanuni hizi unaenda sambamba na matamko mbalimbali yanayotolewa na waandaaji wa maonesho ya Dar es Salaam International Trade Fair (DITF).

## 1.0 FASILI

- 1.1 Neno "Muoneshaji" litajumuisha wafanyakazi, vibarua na mawakala wa kampuni, ubia au ushirika, Shirika lolote, wazalishaji wa nje, au mtu yejote aliyepewa eneo kwa lengo la kufanya maonesho.
- 1.2 "Muoneshaji mdogo" ni kampuni au shirika lolote la ndani/nje linalofanya maonesho katika banda la maonesho sambamba na muoneshaji mkuu.
- 1.3 "Mwandaaji" itamaanisha Mamlaka ya Mandeleo ya Biashara, ambayo humu inatajwa kama TanTrade.

## 2.0 MAOMBI

- 2.1 Maombi lazima yafanyike kwa kutumia fomu rasmi ya maombi inayotolewa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania ambayo itajazwa, kusainiwa kikamilifu na kurudishwa/kutumwa kwa njia ya Posta kwa Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Uwanja wa Maonesho wa Biashara wa Mwl. J. K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, S.L.P. 5402, Dar es Salaam, Tanzania. Nakala moja itarudishwa kwa muoneshaji baada ya kukubaliwa.
- 2.2 Uwasilishaji wa fomu ya maombi haumaanishi kukubaliwa kwa ushiriki katika maonesho hapo baadaye. Kwa kuwasilisha fomu ya maombi,

humaanisha kuwa muoneshaji anazitambua Kanuni hizi na matumizi yake kwake. Vifungu au mashauri yatakayotolewa na upande mmoja kuhusiana na maombi hayatazingatiwa. Pamoja na Kanuni hizi za Ushiriki, Kanuni nyingine zinazotumika nchini kama zitakavyoainishwa na Mamlaka za Tanzania katika eneo la maonesho pia zitahusika kwa kuwa hazikuzingatiwa hapa.

- 2.3 Iwapo kampuni au shirika lolote litashiriki maonesho kuitia wakala wake mkuu au mwakilishi wake wa kitaifa litawasilisha maombi, maombi hayo yaambatane na tamko kwamba wakala huyo mkuu au mwakilishi wa kitaifa amepewa haki pia ya kupanga banda na kuzitangaza bidhaa za huduma zake kwa niaba ya kampuni au shirika hilo.
- 2.4 Maombi ambayo hayatapokelwa kwa wakati yanaweza yasikubaliwe. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Machi. Ili maombi yawewe kushughulikiwa, data zitahifadhiwa, zitatathminiwa na inapobidi zitapelekwa kwa watu wengine wa upande wa tatu kwa lengo la kutekeleza mkataba huu.

### **3.0 KURUHUSIWA KUSHIRIKI KATIKA MAONESHO**

#### **3.1 Masharti ya maonesho**

Maonesho ya silaha, risasi, na milipuko hairuhusiwi kabisa isipokuwa kwa kibali mahususi cha maandishi kutoka mamlaka husika ya Serikali.

#### **3.2 Masharti ya matangazo**

Matangazo ya masuala ya siasa na dini hayaruhusiwi isipokuwa kama kauli husika ya kisiasa/kidini itaendana na maudhui ya maonesho hayo.

#### **3.3 Masharti ya kuingiza nchini Bidhaa za Vyakula kwa ajili ya Maonesho**

- a) Usajili wa muingizaji wa bidhaa pamoja na bidhaa za vyakula zitakazoingizwa nchini;
- b) Maombi ya kuingiza bidhaa hizo kwa kujaza taarifa zinazotakiwa katika fomu zinazohusika;
- c) Vyakula lazima viengizwe nchini kuitia bandari ilioonyeshwa katika fomu;
- d) Ukaguzi wa vyakula katika bandari ya kuingilia utakaofanywa

- na mkaguzi ambaye anaweza kuviruhusu au kuvizua au kupendekeza virudishwe vilikotoka;
- e) Uchunguzi wa kawaida wa kimaabara ili kubaini iwapo vyakula hivyo vinakidhi viwango vilivyowekwa;
  - f) Cheti cha afya kutoka kwa wakala wa udhibiti vyakula na cheti cha uchunguzi;
  - g) Muda wa matumizi uliosalia wa vyakula nya kudumu lazima uwe zaidi ya miezi zita (6) wakati vinapowasili katika bandari ya kuingilia;
  - h) Bidhaa za vyakula zitakazoonekana hazikidhi viwango viliyowekwa katika bandari ya kuingilia zitarudishwa nchi zilikotoka kwa gharama za mwingizaji;
  - i) Matangazo na maelekezo katika vyakula yatahitaji idhini ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ili kuепusha upotoshaji wa taarifa zinazotolewa kwa wateja;
  - j) Bidhaa za vyakula zisizosajiliwa haziruhusiwi kuuzwa kwa wateja;
  - k) Waonyeshaji wote wa bidhaa za vyakula lazima wawe na vibali nya maonesho kutoka TFDA.
- 3.4 Masharti ya kuingiza nchini Bidhaa za Dawa kwa ajili ya Maonesho Muingizaji anatakiwa kuwa:-
- a) Mzalishaji au muuzaji wa jumla wa bidhaa za dawa aliyesajiliwa;
  - b) Idara ya Serikali, mathalani, Idara ya Bohari za Dawa, au vituo nya afya visivyo nya serikali (AZISE – Asasi zisizo za Serikali);
  - c) Shirika/Mtu aliyeidhinishwa anayetoa huduma za vjipimo nya kitabibu nchini na ambaye ana hati ya maadili;
  - d) Mtu aliyeidhinishwa kuingiza dawa nchini kwa masharti maalum kama vile kufanya maonesho;
  - e) Muingizaji wa bidhaa hizi anapaswa kuwasilisha maombi ya kuingiza dawa za maonesho kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) pamoja na Ankara Kifani. Ankara Kifani hiyo lazima ionyeshe aina na kiasi cha bidhaa za dawa zitakazoingizwa nchini kwa ajili ya maonesho. Dawa zote zinazoingizwa nchini LAZIMA zisajiliwe na TFDA au zipewe idhini maalumu kwa ajili ya maonesho;
  - f) Ankara Kifani pamoja na nyaraka nyingine muhimu vitachunguzwa kwa makini na ikiwa zitaonekana zinakidhi masharti yote kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa uingizaji bidhaa nchini, vitaidhinishwa. Hati ya idhni rasmi ya

- g) kuingiza bidhaa hizo nchini itatolewa;
- h) Kabla ya kuruhusiwa, mkaguzi wa dawa anapaswa kukagua kila shehena ya dawa wakati wa kuwasili katika bandari ya kuingilia;
- i) Bidhaa za dawa kwa ajili ya maonesho hazipaswi kuuzwa na katika makasha lazima ziandikwe "HAZIUZWI" au "SAMPULI KWA AJILI YA MATANGAZO";
- i) Maelekezo/Matangazo yatakayotumika wakati wa maonesho lazima yawasilishwe katika Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) angalau wiki mbili (2) kabla ya maonesho ili kuidhinishwa. Huduma hii ni ya bure.

### **3.5 Mabanda ya kuchangia/ubia**

Mabanda ya kuchangia/ubia yanaruhusiwa ili mradi taarifa ya maandishi kutoka kwa makampuni au mashirika yote yanayoshiriki katika mabanda hayo itolewe kwa TanTrade. Bidhaa na huduma zote za maonesho zinazotolewa lazima ziendane na uainishaji wa eneo la maonesho la muoneshaji zikiwa na maelezo ya kutosha (jina na aina, muundo (modeli) katika fomu ya maombi.

### **3.6 Uuzaji au utoaji wa bidhaa**

Uuzaji au utoaji wa bidhaa za vyakula na vinywaji au sampuli unahitaji kibali cha maandishi; TanTrade ina haki ya kuzitwaa bidhaa zinazouzwa bila kibali cha maandishi.

### **3.7 Kushindwa kulipa fedha za ushiriki au kukiuka kanuni za ushiriki**

Waonyeshaji wanaoshindwa kulipa fedha zinazotakiwa na Mwandaaji au watakaokiuka Kanuni za Ushiriki, au kifungu chochote cha sheria wanaweza kuondolewa katika maonesho hata kama maonesho yatakuwa yameanza.

### **3.8 Ukodishaji wa mabanda**

Muoneshaji haruhusiwi kukodisha, kugawa au kuhamisha umiliki wa sehemu au eneo lote alilopanga kwenda kwa mtu mwengine; wala haruhusiwi kumpangisha au kumruhusu mtu mwengine ye yeyote kumiliki au kutumia kwa namna yoyote ile eneo lote au sehemu yake. Bidhaa/huduma na mali halali tu za muoneshaji, au bidhaa na mali ambazo biashara yake inajihuisha nazo ndizo zitakazoruhusiwa kuonyeshwa naye katika eneo lake la maonesho.

### **3.9 Makampuni au mashirika yaliyosajiliwa nchini**

Makampuni au mashirika yaliyosajiliwa nchini Tanzania yataruhusiwa kushiriki kama waonyeshaji wa ndani na yale yaliyosajiliwa kwingineko na/au yanaendesha shughuli zake Tanzania kwa kutumia "Hati ya Uzingatiaji wa Viwango" yataruhusiwa kushiriki kama waonyeshaji wa nje. Ili kushiriki kama muoneshaji wa ndani, kampuni au shirika linaloomba ni lazima litoe nakala ya hati ya usajili.

### **3.10 Maamuzi ya kuruhusu mtu kushiriki**

Uamuzi wa kumruhusu mtu au shirika kushiriki katika maonesho ni wa TanTrade.

- a) Muoneshaji atapokea taarifa ya maandishi ya kuruhusiwa kushiriki na mkataba kati ya muoneshaji na TanTrade utachukuliwa kuwa umekamilika pale fomu ya maombi itakapokuwa imetiwa saini na maofisa wa TanTrade baada ya kuhitimisha kwamba muoneshaji, muoneshaji mdogo, wakala/ mawakala na wafanyakazi wake pia wanahusika na kanuni hizi za ushiriki wakijua kwamba kanuni na masharti hayo ni sehemu ya mkataba unaotajwa.
- b) TanTrade ina haki ya kufuta mgawo wa eneo la maonyesho iwapo eneo hilo liligawiwa kwa kuzingatia ushahidi wa uongo uliopolekea mtu huyo kukubaliwa kushiriki katika maonyesho.

### **3.11 Uthibitisho wa mshiriki**

Muoneshaji atathibitisha kwamba anaridhika kwa madaraka huru ya kuonyesha bidhaa za maonyesho alizozisajili.

### **3.12 Mambo ya kuzingatia wakati wa maandalizi**

Muoneshaji anapaswa kuzingatia kwamba katika kipindi cha maandalizi kuelekea kwenye maonyesho, mabadiliko yanaweza kutokea kuhusiana na mpangilio na mahali ambako mabanda yatawekwa. TanTrade haitawajibika kwa madai yoyote yatakayoelekezwa kwake kutokana na mabadiliko hayo. Ugawaji wa eneo la maonyesho lililoombwa utafanywa na TanTrade kwa kuzingatia bidhaa za maonyesho zilizosajiliwa na uainishaji wa eneo la muoneshaji.

## **4.0 WAONYESHAJI WADOGO**

### **4.1 Maombi ya washiriki wadogo**

Maombi ya waonyeshaji wadogo kuruhusiwa kushiriki katika

maonyesho lazima yatumwe kwa kujaza Fomu Na 2. Ada ya usajili kwa kila muoneshaji mdogo anayeruhusiwa kushiriki katika maonesho ni sawa na asilimia 15 ya gharama za kupanga banda la maonesho. Kiasi hicho cha fedha kitatozwa sambamba na gharama za kupanga banda la maonesho.

#### **4.2 Ushiriki wa makampuni makubwa**

Utaratibu wa malipo, kampuni au shirika halitachukuliwa kuwa ni muoneshaji mdogo iwapo lina ushirikiano wa karibu wa kibiashara na muoneshaji mkuu kama vile kampuni tanzu, kampuni dada, au tawi. Waonyeshaji wadogo lazima wajumuishwe katika orodha rasmi ya waonyeshaji pamoja na anuani zao. Waonyeshaji wadogo wowote watakaojumuishwa katika orodha hiyo ya waonyeshaji bila kibali rasmi watalazimisha TanTrade kuvunja mkataba na muoneshaji huyo na kumfkuza katika maonesho. Muoneshaji atawajibika kulipa fedha anazodaiwa muoneshaji mdogo na atawajibika pia kwa majukumu mengine yanayotokana na Kanuni za Ushiriki.

### **5.0 KANUNI NA MASHARTI YA MALIPO**

- 5.1 Asilimia 100 ya tozo tarajiwa za ushiriki zitalipwa wakati wa kutuma maombi kabla ya tarehe 31 Machi.
- 5.2 Malipo kamili ya tozo za ushiriki ni sharti la msingi la kumiliki eneo la maonyesho, kuingizwa katika orodha ya waonyeshaji, na kupewa aina zote za beji na stika. Malipo ya huduma zingine na mambo mengine yote lazima yafanyike mara moja wakati wa kupokea hati ya madai ya malipo, na kiasi cha ada ya pango lazima kilipwe pamoja na/au bila adhabu/punguzo la bei.
- 5.3 Ikiwa mwombaji ye yote hatatimiza wajibu huo hadi tarehe ya mwisho iliyowekwa, TanTrade ina haki, kwa mujibu wa Kanuni za Ushiriki, ya kumpatia mtu mwengine sehemu iliyokuwa imepangishwa pasipo kumpunguzia mpangaji wa awali wajibu wake. Ikiwa waonyeshaji kadhaa watapanga kwa pamoja banda moja, kila mmoja atawajibika kikamilifu akiwa mmoja wao. Ikiwa muoneshaji hatatimiza wajibu wake wa kifedha kuhusiana na malipo yoyote, TanTrade inaweza kushikilia bidhaa zake za maonyesho na vifaa vyake vya kujengea banda kisha kuviuza kwa mnada wa hadhara katika soko la wazi kwa gaharama za muoneshaji mwenyewe. Vifungu vya sheria vinavyohusiana na ugomboaji wa bidhaa zilizoshikiliwa, kama vinavyotumika, vitaondolewa kwa makubaliano.

## **6.0 USITISHAJI WA MAOMBI/KUTOSHIRIKI**

- 6.1 Inapotokea muoneshaji anasitisha maombi yake baada ya mkatuba kuwa umekamilika, asilimia 100 ya amana iliyolipwa itatwaliwa. Kujiiondoa/kusitisha maombi ndani ya mwezi mmoja wa ufunguzi wa maonesho hakuruhusiwi na gharama zote za ushiriki zinatakiwa kulipwa kikamilifu. Pamoja na gharama kamili za ushiriki, asilimia 100 ya jumla ya gharama zote za ushiriki zinazopaswa kulipwa itatozwa kama adhabu kwa muoneshaji yeьте atakayeshindwa kushiriki maonesho katika banda alilotengewa kwa kipindi chote cha Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.
- 6.2 Inapotokea muoneshaji mdogo akaacha kushiriki, gharama zote za ushiriki lazima zilipwe kikamilifu. Mabanda ambamo wahusika hawatakuwa wameingia ndani ya saa 72 kabla ya maonesho kuanza yatapangishwa kwa watu wengine kwa maslahi ya mwonekano wa jumla wa maonesho. Hata hiyo, muoneshaji anayehusika atawajibika kulipa kiasi chote kilichoonyeshwa katika hati ya madai ya malipo (gharama za ushiriki pamoja na/bila adhabu). Kama hatapatikana mpangaji mwingine kutokana na ufinyu wa muda, upambaji wa eneo pia utafanywa kwa gharama za muoneshaji.

## **7.0 UJENZI NA UPAMBAJI WA MABANDA**

Waonyeshaji wanaopanga maeneo ya kufanya maonesho ya ndani na nje, kwa gharama zao wenyewe, watakuwa na haki ya:

- 7.1 Kujenga mabanda ya maonesho, na
- 7.2 Kuyaweka kwa muundo wanaoutaka ili mradi:-
- Hakuna banda au muundombinu utakaojengwa ndani ya umbali wa mita 3 kutoka njiani/barabarani;
  - Usanifu na maelekezo ya ujenzi yataidhinishwa na TanTrade kabla kazi yoyote ya ujenzi wa banda husika haijaanza, na baada ya kukamilisha ujenzi, banda hilo litakaguliwa na TanTrade na iwapo mamlaka hiyo itajiridhisha kwamba limekidhi viwango, banda hilo litaruhusiwa kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa;
  - Hakuna jengo au muundombinu wowote unaosababisha au wenyе uwezekano wa kusababisha ajali ya moto

- utakaoruhusiwa kujengwa;
- d) Hakuna vyoo binafsi vitakavyoruhusiwa kuwekwa au kujengwa isipokuwa kwa idhini ya maandishi toka TanTrade;
  - e) Hakuna kazi za ujenzi zitakazoruhusiwa wala hapataruhusiwa kuwepo mitambo ya ujenzi, vifaa vya ujenzi, vifusi au masalia ya vifaa vya ujenzi katika eneo la maonesho wakati maonesho yakiedelea bila idhini ya TanTrade.
- 7.3 Wakati kazi ya ujenzi inaendelea, ni lazima kuzingatia nyaya za umeme, mabomba ya maji, vifaa vya usalama, visanduku vya usambazaji, na vitu vingine kama hivyo vilivyopo katika eneo linalohusika. Iwapo vitu hivyo viro katika eneo ambalo mtu amepangishwa, vinapaswa kupewa nafasi ili viwe vinafikika nyakati zote na uharibifu wowote wa vifaa hivyo utakuwa ni jukumu la mpangaji wa eneo/banda husika.
- 7.4 Vifaa vya ujenzi, alama za mabanda na bendera lazima viwekwe kwa namna ambayo haitawaingilia majirani bila sababu ya msingi.
- 7.5 Hairuhusiwi kuweka mazulia kwa gundi katika sakafu za kumbi za maonesho zinazomilikiwa na TanTrade. Inapotokea mtu anakiuka kifungu hiki, TanTrade itasafisha eneo lolote la sakafu ambapo zulia lilibandikwa kwa gundi kwa gharama za muoneshaji na TanTrade itatoa adhabu itakayoona inafaa.
- 7.6 Mapambo na stika za ukutani lazima zithibitike kuwa na sifa za kutoshika moto kirahisi. Matumizi ya vitu kama majani makavu, mabua, nyasi au makuti, au, vifaa vingine vinavyofanana na hivyo hayaruhusiwi. Dari zinazotengenezwa kwa nguo, hata kama hazishiki moto kirahisi, haziruhusiwi kujengwa katika njia za watu au njia za kuijokolea wakati wa dharura.
- 7.7 Vifaa vyovvoste vya ugazi (wa umeme, maji, gesi) vitaruhusiwa kuwekwa baada ya kupata idhini ya TanTrade tu. Vifaa vya kielektroniki vinavyoingiliana na vifaa vya redio au Televisheni/luninga lazima vizimwe mara moja inapotakiwa hivyo na TanTrade.
- 7.8 Muoneshaji atawajibika kwa TanTrade kuhusiana na uharibifu wowote wa majengo na vifaa vilivyowekwa, halikadhalika kuhusiana na uharibifu wowote unaoweza kusababishwa na ujenzi wa banda lake

au bidhaa za maonesho anazoleta.

- 7.9 Moto wa gesi au vifaa vingine vyovypote vya moto, hususan vifaa vinavyotoa joto bila kuunganishwa katika mashine, jenerata, kiyoyozi au vifaa hatari, vitaruhusiwa kutumika kwa kibali maalumu cha TanTrade tu. Moto wa gesi lazima ufuate kanuni za usalama zinazofaa. Vitu vyovypote vinavyoweza kushika moto, kama bomba lolote la ekzosi, au kifaa chochote cha moto lazima viwekwe mbali na moto kama huo, mahali ambapo ni salama. Vifaa hivi vinaruhusiwa pale tu kibali maalum kinapokuwa kimetolewa. TanTrade ina haki na mamlaka ya kuondoa, kwa gharama za muoneshaji husika, chanzo chochote cha moto kisichosajiliwa au kisichoidhinishwa.
- 7.10 Vifaa vya kufungashia visihifadhiwe katika kumbi na mabanda ya maonesho.
- 7.11 Lazima ihakikishwe kuwa vifaa vyote vya usalama na vyumba vya uendeshaji vinapatikana na vinafika kwa urahisi nyakati zote. Upatikanaji na ufikikaji wa vifaa hivi usizuiwe kwa namna yoyote ile. Vifaa au vyumba kama hivyo lazima vitambulike kwa urahisi. Kwa maana hiyo, njia za watu zinachukuliwa pia kuwa ni njia za kuijokolea hata wakati wa vipindi vya ujenzi na ubomoaji.
- 7.12 Ngazi zote au majukwaa yote lazima yafungwe nguzo imara za uzio yaye yanakidhi mahitaji husika ya usalama.

## **8.0 UTANGAZAJI/MABANGO YA MATANGAZO**

Kwa gharama zao, waonyeshaji watakuwa na haki ya kuweka mabango kwenye maeneo yao au kwenye jengo lolote au kwenye muundombini au kuonyesha matangazo au alama sehemu yoyote kwenye maeneo yao, ambayo kwa utashi wa TanTrade ni maelezo ya vitu vinavyozalishwa au bidhaa/huduma zinazotolewa au shughuli zinazofanywa na muoneshaji, ni vya kweli; maelezo yanayotolewa yanaweza kuthibitishwa na TanTrade; hayadhalilishi waonyeshaji wengine, mtu au makampuni; na hayavunji sheria yoyote ya nchi au sera au maadili ya taifa.

TanTrade inaweza kuagiza kuondolewa kwa tangazo au alama yoyote ambayo haizingatii kifungu hiki. Muoneshaji akishindwa kuondoa tangazo au alama ya namna hiyo baada ya kutakiwa kufanya hivyo na

TanTrade, TanTrade inaweza kuliondoa au kuagiza kuondolewa kwa tangazo au alama hiyo kisha gharama zake kulipwa na muoneshaji. Aina yoyote ya utangazaji, mathalani, uendeshaji wa mashine, uonyeshaji wa picha, na maonesho ya sinema utahitaji kibali cha maandishi kutoka TanTrade.

### **Marufuku**

Muoneshaji haruhusiwi kubandika bango, tangazo, mchoro, au vitu vilivyoidhinishwa kwenye jengo au muundombinu wowote na kwenye eneo/maeneo yake kwa namna ambayo itaondoa mwonekano, au vinginevyo, wa eneo la mbele lililotengwa na TanTrade. Ni marufuku kwa muoneshaji yeoyote kubandika bango, tangazo, mchoro, au vitu vingine kwenye jengo au vitu vingine vinavyomilikiwa na TanTrade bila idhini na katika mazingira yale tu ambayo yataruhusu.

## **9.0 WAJIBU WA WAONYESHAJI**

- 9.1 Wakati wote kuweka maeneo yao katika hali ya usafi na unadhifu na/ au kuhakikisha kuwa yanasa fishwa na kuwa tayari kila asubuhi kabla ya saa za ufunguzi wa maonesho.
- 9.2 Kuzingatia sheria ndogondogo za Jiji la Dar es Salaam.
- 9.3 Kukamilisha upangaji wa bidhaa za maonesho/huduma na kuwa tayari angalau saa 42 kabla ya ufunguzi wa maonesho.
- 9.4 Kuwekeea bima bidhaa/huduma wakati zinapoletwa katika eneo la maonesho, wakati wa maonesho, na wakati zinapoondolewa kutoka Uwanja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.
- 9.5 Kuweka vifaa vya kuzimia moto kwenye banda.
- 9.6 Kuheshimu Haki ya Mali za Viwanda (haki miliki ya kisheria, haki miliki na nembo ya kibiashara) ya waonyeshaji wengine, na kujizua kukiuka sheria hizo. Ikiwa na ushahidi wa ukiukwaji wa sheria ya mali ya viwandani, TanTrade itamtaka mhusika kuacha mara moja ukiukaji huo wa sheria na, kama agizo hili halitatekelezwa mara moja, TanTrade itaondoa bidhaa/huduma au mchoro huo kutoka sehemu husika, au kufunga banda la muoneshaji. Vilevile, TanTrade ina haki ya kumzuia mvunja sheria kuingia/kushiriki katika maonesho yatakayofuata au kumruhusu kushiriki katika maonesho kwa masharti, wajibu, na

dhamana maalum. Hata hivyo, kifungu hiki hakilazimishi TanTrade kuchukua hatua kuhusiana na ukiukaji wa haki miliki ya viwanda na hakuna uwezekano wa kutoa madai dhidi ya TanTrade.

## 10.0 MASHARTI YA UUZAJI/MAUZO

Mauzo ya moja kwa moja yanaruhusiwa katika maeneo yaliyotengwa maalum.

Mauzo kwa fedha taslimu katika kaunta na kwa huduma na bidhaa nyingine unaruhusiwa kwenye mabanda; eneo litakalotumiwa kwa madhumuni haya halitazidi asilimia 20 ya eneo la maonesho lilitotolewa.

## 11.0 MARUFUKU MAALUM

Hakuna muoneshaji atakayeruhusiwa:

- a) Kukata/Kuharibu mti/miti au uoto kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka TanTrade.
- b) Kutumia eneo au jengo au muundombinu wowote kwa namna itakayosababisha uharibifu au usumbufu kwa watu, TanTrade, waonyeshaji, au watumiaji wa maeneo mengine.
- c) Kugawa machapisho au vipeperushi vyta matangazo au kitu chochote sehemu yoyote ndani ya uwanja wa maonesho nje ya eneo lake isipokuwa kwa kibali cha maandishi kutoka TanTrade.
- d) Kuuza bidhaa, ama kwa jumla au rejareja, kutoka kwenye banda lake isipokuwa kwa kibali maalum cha maandishi kutoka TanTrade na isipokuwa kwa bidhaa na kwa masharti yale tu kama itakavyoolezwa na TanTrade. Kifungu hiki hakizuij kupokea oda ya bidhaa au huduma kutoka nje ya Uwanja wa maonesho.
- e) Kuendesha shughuli au biashara yoyote tofauti na maonesho ya bidhaa na huduma ambazo muoneshaji anahusika au anatengeneza, na kupokea oda ya usambazaji wa bidhaa/ huduma hizo sehemu nyingine nje ya uwanja wa maonesho isipokuwa kwa kibali maalum cha maandishi toka TanTrade.
- e) Kupiga muziki.

## **12.0 UKOMO WA DHIMA YA TANTRADE**

Wakati wowote TanTrade haitahusika na upotevu/hasara, uharibifu wa aina yoyote uliompata au uliofanywa na muoneshaji, wafanyakazi, vibarua, wakandarasi, wakala au wageni wake kutokana na sababu yoyote, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa jumla wa miundombinu, majengo au mitaro, uharibifu au kushindwa kusambaza maji, umeme, au huduma nyingine, moto, mafuriko, wizi, uharibifu, ugaidi, au matukio ya vita au matukio yaliyo nje ya uwezo wa TanTrade.

## **13.0 UWEKAJI WA HUDUMA ZA MAWASILIANO YA SIMU**

Muoneshaji anaweza, kwa maombi maalum, kuwekewa huduma ya muda ya mawasiliano ya simu kutoka kwa mto huduma ye yeyote atakayependekezwa na TanTrade. Muoneshaji atalipa gharama za huduma hiyo ya simu moja kwa moja kwa mto huduma husika.

## **14.0 UONDOAJI WA BIDHAA, MAJENGO, NA MIUNDOMBINU YA MAONESHO**

- a) Waonyeshaji wataondoa bidhaa zote za maonesho kutoka kwenye uwanja wa maonesho na kubomoa miundombinu yote katika maeneo yao ya maonesho ndani ya siku mbili baada ya kufungwa kwa maonesho. Muoneshaji pekee ndiye mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa anaondoka kwenye mabanda ya maonesho kwa wakati. Mara baada ya muda wa kuondoa mabanda kwisha, makubaliano yote kati ya pande mbili yatakoma. Usalama wa bidhaa au vifaa vyovoyote vya majengo au kitu chochote ambacho kitaendelea kuwepo kwenye mabanda/kumbi za maonesho baada ya muda huo utakuwa ni jukumu la muoneshaji mwenyewe.
- b) Funguo za mabanda zinapaswa kukabidhiwa kwa TanTrade ndani ya saa 72 baada ya kufungwa kwa maonesho. Kushindwa kutekeleza kanuni hii, muoneshaji atalipa kila siku faini ya asilimia 10 ya kodi ya pango ya mwaka ya Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam.
- c) Bidhaa zozote za maonesho na vifaa vya ujenzi wa mabanda ambavyo vitakuwa havijaondolewa ndani ya siku saba (7)

- baada ya kufungwa kwa maonesho, vitachukuliwa kuwa vimetekelizwa na waonyeshaji, hivyo TanTrade itaviteketiza kwa namna itakayoona inafaa kwa gharama za muoneshaji.
- d) Kabla muda rasmi wa ubomoaji kuanza, waonyeshaji hawaruhusiwi kuondoa bidhaa zozote za maonesho kutoka kwenye mabanda yao au kuanza kubomoa mabanda. Katika hali ya ukiukaji wa kanuni hii, TanTrade ina haki ya kutoa adhabu ya faini ya Dola za Marekani 2,000 au kiasi sawa na hicho kwa sarafu ya Tanzania.

## 15.0 ORODHA YA MAJINA YA WAONYESHAJI

Kila muoneshaji, kuitia maombi yake, anapaswa kukubali majina ya kampuni na waonyeshaji wake wadogo kuingizwa kwa mfuatano wa alfabeti katika orodha ya majina ya waonyeshaji. Ni waonyeshaji na waonyeshaji wadogo rasmi tu ndio watakaoorodheshwa katika kitabu cha orodha ya waonyeshaji. Ikiwa taarifa inayohitajika kwa ajili ya uingizaji wa lazima katika kitabu cha orodha ya waonyeshaji hazikutolewa kwa wakati, majina yataingizwa kwa kuzingatia taarifa zilizopo. Hakutakuwa na madai ya kisheria yatakayotolewa kutokana na majina yasiyo sahihi, yasiyokamilika, au yaliyokosekana.

## 16.0 VITEGAUCHUMI NDANI YA UWANJA WA MAONESHO

Vitegauchumi ndani ya Uwanja wa Maonesho husimamiwa kwa sheria na kanuni tofauti. Sambamba na hizo, kanuni zifuatazo zitatumika kuhusiana na wamiliki wa kudumu wa mabanda:-

### 16.1 Pasipo na Ushiriki wa Wamiliki wa Mabanda

- a) Pale ambapo wamiliki wa mabanda hawatashiriki katika matukio/maonesho yoyote yaliyoandaliwa na TanTrade na kufanyika katika maeneo yao, wamiliki hao wa mabanda wanapaswa kukabidhi maeneo/mabanda yao ya maonesho kwa TanTrade miezi mitatu kabla kwa matumizi bora na kwa manufaa ya jumla ya maonesho. Eneo/Banda litakabidhiwa tena kwa mmiliki mara tu baada ya kufungwa kwa maonesho. Kutoshiriki kwa miaka mitatu mfululizo kutamaanisha kutwaliwa kwa umiliki wa banda.
- b) Muoneshaji yejote anayetaka kufanya marekebisho/

kuboresha eneo/banda la kupanga atapaswa kuomba kibali kutoka TanTrade. Ikiridhishwa na marekebisho/maboresho yaliyopendekezwa, TanTrade itamruhusu muoneshaji kuanza marekebisho/maboresho kwa gharama zake mwenyewe. TanTrade haitapokea maombi ya punguzo la kiwango cha malipo kutokana na gharama zilizotokana na marekebisho au maboresho yaliyoidhinishwa. Hata hivyo, muoneshaji atapewa kipaumbele wakati wa ugawaji wa mabanda iwapo atataka kutumia eneo/banda hilohilo alifofanya marekebisho/maboresho yaliyofanyika yataachwa hivyo hivyo baada ya kufungwa kwa maonesho.

## **16.2 Kuziba Njia/Maeneo ya Wazi**

Hakuna muoneshaji, wakati wowote ule, kwa kutumia bidhaa zake au kwa namna nyingine yoyote ile, atakayeruhusiwa kuziba barabara, njia, au eneo la wazi. Ukiukaji wa kanuni hii utaipa TanTrade haki ya kuondoa kizuizi hicho kwa gharama za muoneshaji iwapo muoneshaji husika atashindwa kuondoa kizuizi hicho ndani ya dakika 60 baada ya kutakiwa kufanya hivyo na TanTrade.

## **16.3 Uwekaji Uzio Mashine**

Mashine zote zinazosogea zinapaswa kuwekeza uzio au kingo na sehemu zote zinazosogea kujengewa vizuri kwa namna ambayo itazuia majeraha kwa watu.

## **16.4 Bidhaa Hatari, Zinazochukiza, na za Kelele**

- a) TanTrade, kwa utashi wake, inaweza kumuagiza muoneshaji kuondoa bidhaa yoyote ya maonesho ambayo kwa maoni yake ni hatari.
- b) Kila itakapoona ni muhimu, kwa maslahi ya afya, faraja, na usalama wa watu, TanTrade inaweza kuweka sheria na kanuni kuhusiana na bidhaa za maonesho zinazoudhi au za kelele au zinazoweza kusababisha usumbufo.
- c) Hakuna muoneshaji atakayeweka au kutumia mifumo ya kupazia sauti ndani na nje ya eneo lake isipokuwa kwa kibali maalum kutoka TanTrade.
- d) Waonyeshaji wa radio, kaseti, televisheni/luninga, vifaa vya kurekodi sauti, na vifaa vingine kama hivyo wanapaswa kuhakikisha kuwa viwango vya sauti zinazozalishwa hazisababishi kelele kwa waonyeshaji wengine na kwa watu wengine wanaotembelea Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. TanTrade ina haki ya kutekeleza kanuni inayohusiana na matumizi ya vifaa/vyombo hivyo na viwango

vya kelele zinazozalishwa na vyombo/vifaa hivyo, kadri itakavyoona inafaa.

### **16.5 Fidia**

Muoneshaji atawajibika kufidia TanTrade kwa hasara/upotevu, uharibifu, au madai yoyote na gharama za utetezi/malipo ya madai yanayotokana na:-

- a) Ukiukwaji wa Kanuni za Ushiriki au kitendo chochote, ukwepaji, au upuuzaji unaofanywa na muoneshaji, wafanyakazi/vibarua, wakandarasi, wakala, washirika wake; au
- b) Ikiwa ni matokeo ya majeraha au ajali iliyosababishwa na bidhaa za maonesho, mashine, majengo, au miundombinu inayomilikiwa, iliyokodiwa, au iliyozimwa na muoneshaji au kutokana na uwepo wowote wa kitu ambaa muoneshaji anawajibika nao.

### **16.6 Anuani ya Bidhaa za Maonesho zinapoletwa katika Uwanja wa Maonesho**

Bidhaa zote zitakazoonyeshwa katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam zitumwe kwa anuani ya Muoneshaji, c/o Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu J. K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam, na gharama zote zilipwe na muoneshaji mwenyewe. Wakandarasi wote walioajiriwa na waonyeshaji kwa ajili ya ujenzi wa majengo na miundombinu kabla ya Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kuanza wanapashwa kuelekeza vifaa vyao vyote kwa Muoneshaji, c/o Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania.

### **16.7 Uingiaji Ndani ya Uwanja wa Maonesho kabla ya Ufunguzi wa Maonesho**

Kibali cha kuingia ndani ya Uwanja wa Maonesho kabla ya ufunguzi wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kitatolewa na TanTrade. Waonyeshaji na/au wakandarasi, mafundi, na wafanyakazi wao waliodhinishwa watapata kibali hicho kutoka katika Ofisi za Utawala za Maonesho ya Biashara. Kibali hicho kitamruhusu mhusika kuingia Uwanjani wakati wowote ndani ya saa za kawaida za kazi kwa ajili ya ujenzi/uwekaji wa miundombinu kama itakavyohitajika ili kuhifadhi bidhaa zao za maoneshoo. Uingiaji utafanyika kwa kutumia milango itakayoamuliwa na TanTrade.

## **16.8 Upakaji Rangi wa Kuta**

Hakuna muoneshaji atakayeruhusiwa kuchora, kupaka rangi inayofutika, au rangi nyingine yoyote au kubadilisha umbo la ndani la ukuta wowote wa banda lolote bila ya idhini ya maandishi kutoka TanTrade, au kusababisha uharibifu wa aina yoyote kwenye mali za TanTrade. Uharibifu wowote utakaosababishwa na vitendo hivyo utafidiwa na muoneshaji husika na kwa hali hiyo TanTrade kwa utashi wake ina haki ya kuagiza kufanyika kwa ukarabati wa uharibifu huo na gharama zitakazotokana na ukarabati huo kulipwa kikamilifu na muoneshaji husika.

## **16.9 TanTrade Itakuwa na haki ya:**

- a) Kuzuia uingiaji ndani ya Uwanja wa Maonesho wakati wowote au wakati wa tukio lolote mahususi.
- b) Kutoza viingilio ndani ya Uwanja wa Maonesho kadri itavyoona inafaa.
- c) Kupitia wawakilishi na wafanyakazi wake waliodhinishwa, kuingia ndani ya eneo au jengo, au muundombinu wowote kwa lengo la kukagua na kutekeleza jukumu lolote kutokana na ulazima au kama itakavyoonekana inafaa.
- d) Kupitia wawakilishi au wafanyakazi wake waliodhinishwa kujenga, kuweka, kukagua, kukarabati na kutengeneza mabomba, nyaya za umeme, na seva juu au chini ya eneo lolote la wazi ilimradi tu kwa kufanya hivyo kutaondoa tatizo lililokuwa limesababishwa na uharibifu katika mali ya muoneshaji.
- e) Kufuta maonesho, kubadili tarehe, mahali, au wakati wa maonesho ikiwa itahitajika kutokana na mazingira maalum, amri ya polisi, au sababu nyingine ambazo TanTrade itaziona ni muhimu.
- f) Kubadilisha eneo/banda/jengo alilopangiwa muoneshaji pasipo kuwajibika kwa uharibifu, madai ya kupunguziwa kiwango cha malipo au fidia ambayo imetokana na mabadiliko hayo na/au iwapo muoneshaji atashindwa kuendeleza umiliki wa eneo/banda ndani ya muda ulioainishwa. Mabadiliko hayo hayatampa muoneshaji haki ya kujitoa kwenye mkataba wa ukodishaji.
- g) Kumtaka muoneshaji kutoa taarifa zinazohusiana na mamlaka ya biashara yake iliyofanyika wakati wa maonesho. Taarifa hizo zitatumwiwa na TanTrade kwa madhumuni ya tathmini.

## **16.10 Magari katika Uwanja wa Maonesho**

Ni magari yaliyoidhinishwa tu ndiyo yanayoweza kuingizwa ndani ya

Uwanja wa Maonesho. Magari yaliyoidhinishwa yanapaswa kuegeshwu katika maegesho ya magari yaliyotengwa. Ulinzi na Usalama wa magari yote yaliyoingizwa ndani ya Uwanja wa Maonesho ni jukumu la wamiliki wa magari husika. TanTrade ina haki ya kuliondoa gari lolote liloingizwa ndani ya Uwanja wa Maonesho ikiwa limeegeshwa visivyo au limeingizwa ndani ya Uwanja wa Maonesho bila idhini ya TanTrade, kasha gharama zake kulipwa na mmiliki wa gari husika.

### **16.11 Uahirishaji wa Maonesho**

Maeneo/Mabanda yote yatakodishwa kwa sharti kwamba ikiwa maonesho yataahirishwa au kufutwa kutoptaka na sababu zilizo nje ya uwezo wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania, TanTrade haitahusika na hasara iliyotokana na uahirishaji wa ufutaji huo. TanTrade haitawajibika kurejesha tozo na ada zilizokwishalipwa.

## **17. MISINGI YA MIKATABA NA KANUNI ZA NYONGEZA**

Pamoja na Kanuni hizi za Ushiriki, kanuni na vifungu vya kiuratibu (mathalani, taarifa za muoneshaji) au kiufundi (mathalani, miongozo ya mitindo ya mabanda) au vifungu vingine vyovyyote vya wamiliki wa Uwanja wa Maonesho ambavyo muoneshaji huvipokea kabla ya kuanza kwa maonesho vitachukuliwa kuwa ni sehemu muhimu ya misingi ya mkataba unaosimamia ushiriki katika maonesho haya.

## **18. MAREKEBISHO**

TanTrade ina haki ya kipekee kuongeza, kubadili, au kufuta kanuni yoyote kati ya Kanuni hizi za Ushiriki. Mabadiliko yoyote ya Kanuni hizi za Ushiriki yataanza kutumika mara moja kuanzia tarehe zilipobandikwa na TanTrade. Uamuzi wa Bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania yatakuwa ya mwisho kuhusiana na masuala yote yatakayohusisha TanTrade na waonyeshaji kuhusiana na tafsiri au maana ya Kanuni hizi za Ushiriki.

## **19. UTEKELEZAJI WA KANUNI ZA USHIRIKI**

Kanuni na masharti ya makubaliano ya biashara yoyote yaliyofanywa na TanTrade yatakuwa sawa na haya na yatasimamiwa na Kanuni hizi za Ushiriki. Watu wote wenye ofisi ndani ya TanTrade, wafanyakazi wa TanTrade, na watu wengine kama walivyoidhinishwa na TanTrade

wana madaraka/dhamana ya kusimamia utii na uzingatiaji madhubuti wa Kanuni hizi za Ushiriki.

## **20. UKIUKAJI WA KANUNI ZA USHIRIKI**

Kuhusiana na ukiukaji wa Kanuni yoyote ya Ushiriki unaofanywa na muoneshaji pamoja na kanuni nyingine zozote za kisheria zilizopo, TanTrade, kwa utashi wake, ina haki ya:-

- 20.1 Kufuta maombi ya eneo na iwapo muoneshaji tayari ni mmiliki wa eneo, kumuondolea umiliki. Katika hali hiyo, TanTrade ina haki ya kutorejesha ada ya pango iliyokwishalipwa, ikiwa ni madhara ya uvunjaji wa Kanuni hizi za Ushiriki; muoneshaji na TanTrade wanakubaliana kwamba ada iliyolipwa ni kiasi kinachotosha kulipia uharibifu ambao TanTrade imeupata ikiwa ni matokeo ya ukiukaji huo. Ikiwa Jengo au muundombinu umejengwa katika eneo ambalo halikuruhusiwa, jengo au muundombinu huo utatwaliwa na TanTrade bila malipo ya fidia?????. Ikiwa jengo au muundombinu wowote hautahitajiwa na TanTrade, jengo au muundombinu huo utaondolewa, ambapo kwa hali yoyote ile gharama za uondoaji zitalipwa na muoneshaji.
- 20.2 Kumtaka muoneshaji kurekebisha uharibifu, na anaposhindwa kutekeleza agizo hilo, kurekebisha uharibifu kisha gharama za marekebishi kulipwa na muoneshaji.
- 20.3 Kudai malipo ya uharibifu uliotokana na ukiukaji wa mkataba.

## **21. USIRI / FARAGHA**

TanTrade itazishughulikia siri zote za kibiashara itakazozijua wakati wa maonesho kwa faragha kubwa.

## **22. MIGOGORO**

Migogoro inayotokana na mikataba itatatuliwa kiungwana na ikishindikana, mgogoro utaamuliwa kupitia Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye dhamana ya kushughulikia shauri husika.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na

**Mkurugenzi Mkuu**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania  
Viwanja vya Maonesho vya Mwl. J. K. Nyerere, Barabara ya Kilwa,  
S.L.P 5402,  
DAR ES SALAAM, TANZANIA.  
Simu: +255 22 2850 238,  
Nukushi: +255 22 2850 239/539  
Barua pepe: [info@tantrade.or.tz](mailto:info@tantrade.or.tz)  
Tovuti: [www.tantrade.org](http://www.tantrade.org)